

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

LEARNING BY EAR 2010

SHALL I TELL YOU SOMETHING?

AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 03: LIPUA LIPUA

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAÏMA GUIRA**

TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS

PROOFREADING: TONY DUNHAM

KISUAHELI: ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (male, about 40 years old)
2. LIPUA, THE LITTLE PIGEON (female, 15-20 years old)
3. OTHER BIRDS (3 or 4 fem. voices, can also be spoken by narrator)
4. NINKI NANKA THE SNAKE (female, about 20 yrs old)
5. SIMBA THE LION (male, about 30 years old)
6. KARAMBA THE KING (male, about 40 years old)
7. 2 GUARDS (male, age irrelevant)

INTRO/ PRESENTER:

Hujambo na karibu kwa makala ya tatu katika mfululizo wa vipindi vyetu vya "Noa Bongo! Jenga maisha yako" bado tukiwa katika masuala ya ngano, maada kuu ikiwa ni "JE, NIKUDOKEZEE?" Hizi ni ngano kuhusu utamaduni wa Mwfrika katika kudumisha amani na maadili mema mionganoni mwa jamii.

Maudhui ya ngano hizi kuhusu wanyama ni kuweka wazi ukweli wa mambo katika jamii. Ni ngano za kusisimua hasa mionganoni mwa watoto na pia hutumiwa kuelezea mienendo au maisha ya

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

mwanadamu. Aidha ngano hizi zinaangazia zaidi mizozo na jinsi inavyoweza kutatuliwa kwa amani na kuleta maridhiano. Unaposikiliza kwa makini hukosi kujifunza jambo moja au mawili ambayo yanaweza kukusaidia maishani. Mfano ni jinsi kiumbe dhaifu kinavyoweza kupata umaarufu, au jinsi wanyonge wanavyoweza kupata uwezo mkubwa. Endelea kuwa nasi hadi mwisho ujifunze mengi katika kipindi hiki kuhusu njiwa mjasiri kwa jina “**LIPUA LIPUA**”.

1. MUSIC (play as background for the entire script)

2. NARRATOR:

Zamani za kale palitokea mfalme mmoja mlafi na habithi kwa jina Karamba. Kwa ulafi wake mfalme huyu bila ya hata kuona haya aliwanyang'anya maskini mali na mazao yao. Na hali ikawa mbaya kiasi cha ndege kuanza kufariki kutokana na ukosefu wa chakula. Kufuatia janga hilo, m Kutano mkubwa ukaitishwa kuzungumzia suala hili.

Kwa jinsi walivyokuwa wameathirika na njaa, ndege hao waliamua kufika mbele ya mfalme kutoa malalamishi yao. Lakini nani mionganoni mwao angeweza kujitokeza nani kumweleza mfalme malalamishi hayo?

3. SFX : *Birds chirping*

4. NARRATOR:

Hakuna?

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

5. LIPUA THE PIGEON (*after a while, in a small voice*):

“Mimi hapa nitamweleza!”

6. NARRATOR:

... akajitokeza Njiwa mdogo sana kwa jina “Lipua”, huku akikukuma kukuma kwenye mkusanyiko huo.

7. LIPUA THE PIGEON:

“Nitaenda.”

8. NARRATOR:

Ndege wengine wote wakamshangaa!

9. SFX: *Nervous fluttering of bird's wings*

10. OTHER BIRDS:

“Wewe una wazimu! Karamba atakushika na kukutafuna tafuna!”

11. NARRATOR:

... Ndege wote wakamtahadharisha! Lakini kwa sababu hakuna mwingine aliyejitokeza, wakaridhia wazo lake. Na asubuhi na mapema Lipua akafunga safari kwenda kwa mfalme.

12. SFX: *Fluttering of bird's wings*

13. NARRATOR:

Moyo ulimdunda! Hasa kwa kuzingatia kwamba ndege wote walikuwa wamemtahadharisha dhidi ya kusimama mbele ya

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

Mfalme Karamba.

14. LIPUA THE PIGEON:

“Lakini hakuna jinsi lazima mmoja wetu ajitokeze kukabiliana na ubabe wa mfalme huyu kuokoa ndege wengine wasife kutokana na baa la njaa.”

15. NARRATOR:

...Lipua akajipa moyo....

16. SFX: *Fast fluttering of bird's wings*

17. LIPUA THE PIGEON: *panting*

18. NARRATOR:

Na alipotua kwenye tawi la mbuyu huku akihema kwa woga, Lipua alisikia sauti ya nyoka mwenye sumu kali kwa jina Ninki Nanka, ikitoka kichakani chini ya mbuyu huo.

19. NINKI NANKA THE SNAKE: *hissing*

20. NINKI NANKA THE SNAKE:

“Kwanini unahema hivyo, Lipua? Kwani una haraka ya kwenda wapi asubuhi hii?”

21. LIPUA THE PIGEON:

“Oh! Naenda kukutana na Mfalme Karamba”

22. NARRATOR:

Na kwa masikitiko akaanza kumweleza Nyoka yote yalitotokea. Ninki Nanka alimsikiliza kwa makini na kisha mara moja akatoa kauli yake.

23. NINKI NANKA THE SNAKE:

“Una habari? Sasa mimi nitaandamana nawe hadi kwa mfalme. Huyu mfalme amewaua wenzangu wengi sana kisha kuwachuna ngozi na kuzitumia kama vazi na talasimu. Labda kutokana na

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

ushirikiano wetu tunaweza kumshinda.

24. NARRATOR:

Kwa furaha Lipua alikubaliana naye na akumwambia ajifiche chini ya mbawa zake. Kisha wakaelekea kwa mfalme. Hata hivyo haikuwa rahisi kwa Lipua kupaa kutokana na uzito wa Nyoka, lakini akajikakamua hadi wakafika kwa mfalme. Punde tu walipotua katika kichuguu kimoja cha mchwa, Simba ambaye alikuwa akirandaranda karibu na makao hayo, alimuita kwa sauti ya kuogofya:

25. SIMBA THE LION roars

26. SIMBA THE LION:

“Lipua, mbona unahema hivyo? Kwani unafukuzwa na mashetani ?”

27. LIPUA THE PIGEON:

“Oh hapana ! Niko mbioni maana nimekabidhiwa jukumu la kukutana na kuzungumza na Mfalme Karamba.”

28. NARRATOR:

Na bila kupoteza wakati akamhadithia Simba yote yalitoyokea.

Kisha Simba akasema:

29. SIMBA THE LION:

“Mimi pia nina kisasi na huyo Mfalme Karamba. Amewaua wenzangu wengi na kutumia ngozi na mafuvu ya vichwa vyao kurembesha makao yake. Hebu panda mgongoni mwangu nikupeleke”.

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

30. NARRATOR:

Kwa furaha, Lipua, akapanda mgongoni mwa Simba huku Nyoka
akiwa chini ya mbawa zake na kuanza safari ya kwenda nyumbani
kwa mfalme. Walifika kwa wakati ufaao kabisa sawia na
wafanyibishara ambao kwa kawaida hufika kuwasilisha vyakula na
bidhaa nyingine kwa mfalme. Simba akaketi katikati ya
wafanyibiasha hao huku akinguruma kwa kishindo, naye Lipua
akatua langoni karibu na sehemu inayotengewa walinzi wa mfalme.

31. LIPUA THE PIGEON:

“Tafadhali naomba kumuona mfalme? Nahitaji kuzungumza naye”

32. ALL: *Burst of mocking laughter of 2 to 4 people (played by the actors)*

33. NARRATOR:

Walinzi hao walimcheka kwa kejeli na kisha kumjibu:

34. GUARDS (mockingly):

“Kinyang’arika kama wewe? Umepata wapi ujasiri wa kukutana na
mfalme? Mfalme atakukatakata na kukufanya kitowe!”

35. LIPUA THE PIGEON:

“Tafadhali nipisheni, mimi sina muda wa kusubiri.”

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

36. NARRATOR:

Kwa mshangao, walinzi hao walimuonyesha njia inayoelekea kasri ya mfalme. Lipua alilingiwa na woga lakini akajipa moyo. Walinzi wakimchekelea huku wakielekeza macho na fikra zao zote kwa Njiwa huyo. Wakati hayo yakijiri, Simba na Nyoka walipata fursa ya kujipenyeza bila ya hata kuonekana na walinzi hao. Mfalme Karamba alikuwa ameketi kwenye kitit chake cha enzi raha mstarehe huku meza ikiwa imeja aina ya vyakula. Na kabla hajaanza kula, njiwa akatua kando ya sahani yake.

37. LIPUA THE PIGEON: cooing

38. LIPUA THE PIGEON:

“Amani iwe nawe Mfalme!”

39. NARRATOR:

Kwa mshangao, mfalme Karamba alirejesha kitit nyuma na kujishika kiuno.

40. LIPUA THE PIGEON:

“Mfalme niwie radhi, umaskini umekithiri hapa kwetu na yote ni kwa sababu yako. Wewe unaishi maisha ya raha mustarehe, watu wako wanakufa njaa.”

41. NARRATOR:

Kwa hasira, mfalme alianza kung'ata vidole vyake kwa dharau.

42. SFX: snapping fingers (*played by actors*)

43. NARRATOR:

Na ghafla walinzi wawili wakatokezea.

44. KING KARAMBA:

“Hebu mkamateni haraka huyu ndege! Yaani hiki kinyang’arika

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

hakina adabu kinakuja kunidhihaki wakati nakula chakula! Hebu
mfungieni huko kizimbani na mumpe chakula ashibe. Na kisha
tutamchinja na kumfanya kitoweo.”

45. NARRATOR:

Lipua akakamatwa na kuwekwa kizimbani. Kilichofuatia ilikuwa kazi
rahisi ya kumlisha kwani alikuwa amedhofika kutokana na njaa.

Baada ya siku chache, Njiwa alinona. Siku moja jioni Mfalme
Karamba akawatuma vijakazi wake.

46. KING KARAMBA:

“Hebu mlete yule ndege. Nimetamani sana kula nyama ya njiwa.”

47. NARRATOR:

Basi bila ya kupoteza muda walikwenda moja kwa moja hadi
kizimbani anakohifadhiwa Njiwa. Lakini cha kustaajabisha ni
kwamba, wakati walipojaribu kutia mkono kumtoa Njiwa huyo,
walishtuka kumuona Nyoka Ninki Nanka aliyemuumma mfanyakazi
mmoja. Sumu kali ya Nyoka ilimuathiri haraka mfanyi kazi huyo na
kuanguka papo hapo akafa. Baada ya kusubiri kwa muda, Mfalme
Karamba alimtuma mfanyakazi mwengine. Lakini alipokaribia
kizimba, alikumbana na makali ya Simba.

48. *SOLDIERS cry*

49. *SIMBA THE LION roars + strikes with his paw*

50. NARRATOR:

Mfalme Karamba ambaye wakati wote alikuwa akisubiri
wafanyakazi wake wamlete Njiwa, alianza kuwa na wasiwasi.

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

51. KING KARAMBA:

“Mbona wanakawia hivi, hawa wafanyakazi wangu pia nitawafunza adabu, ehhhh... watanijua mimi ni nani!”

52. NARRATOR:

Kwa hasira Mfalme Karamba aliondoka pole pole kwenye kitit chake cha enzi na kuelekea moja kwa moja hadi kwenye lile tundu anakohifadhiwa Njiwa.

53. KING KARAMBA:

“Sasa kwa kuwa muwakaidi nitawafunza adabu ”

54. NARRATOR:

Kisha maneno yakamsakama kwa mshtuko wa kuwaona wafanyakazi wake warefu, wajasiri na wenye nguvu wakiwa wamelala sakafuni huku tundu la Njiwa likiachwa wazi.

55. LIPUA THE PIGEON: *cooing*

56. NARRATOR:

Lipua alikuwa akiruka ruka na kuimba kwa furaha kwenye tundu lake. Mfalme Karamba hakuamini macho yake.

57. KING KARAMBA:

“Hii ni kazi ya shetani”

58. NARRATOR:

...Alishtuka na kuwaza huku akitetemeka kwa hofu. Alimtazama Lipua kwa hofu na kumfananisha na mchawi, kutokana na miujiza aliyojionea. Kwa hofu alikusanya vitu vyake vyote, mbio akaanza kutoroka asirudi tena.

Baadaye mkutano uliitishwa kumchagua kiongozi mnyenyeketu

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 03 Lipua-Lipua

Author: Ibrahima Ndiaye

kuchukua mahala pa mfalme. Na jukumu lake la kwanza lilikuwa kurejesha mali yote iliyoporwa na Mfalme Karamba. Sherehe kubwa ikaandaliwa na kila mmoja aliiimba na kucheza kwa furahia usiku kucha.

59. MUSIC

60. NARRATOR:

Tangu siku hiyo, wanyama hao huandaa sherehe kila mwaka kwa heshima ya Nyoka Ninki Nanka, Simba, lakini zaidi kwa ujasiri wa Njiwa Lipua.

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na atajaye kuwa wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.

OUTRO / PRESENTER:

Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa ngano yetu LIPUA LIPUA. Je, maoni yako ni yapi kuhusu ngano hii? Umewahi kushuhudia mtu anayejinyima na kujitolea, kisha mwishowe akapindukia kuwa shujaa? Tuandikia kuititia email yetu lbe@dw-world.de au ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki na vingine vya Noa Bongo, tembelea mtandao wetu www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa.

END